KUJIFUNZA KUHUSU UONGOZI
Mwongozo wa Kujifunza kwa Kushiriki

Tunawahimiza kuwa katika vikundi na kujadili maudhui kwa namna itawayowafaa zaidi.

Kujifunza Kuhusu Uongozi:

- **Kestoria 3: Wanawake Walioshika Usukani: Simulizi za Ujasiri, Uthubutu, na Mafanikio** Ikiangazia wanawake Madiwani watatu kutoka mkoa wa Morogoro. Yapo kwa Kiingereza na Kiswahili
- **Makala Nne za Video** zenye simulizi za Wanawake Walioshika Usukani. Yapo kwa Kiswahili.
- **Makala za Sauti** yenye simulizi za Wanawake Walioshika Usukani.Yapo kwa Kiswahili.
- **Maigizo Matatu za Video** kuhusu ushiriki wa wanawake katika uongozi. Yapo kwa Kiswahili.
- **Nyimbo Tatu** kuhusu ushiriki wa wanawake katika uongozi.

Tunaimani kuwa mtafurahia kusoma vitabu na kuangalia video kutoka TGNP, na pia kuwashirikisha wengine. Maudhui haya yanapatikana bure kwa ajili ya kusoma, kusikiliza, au kuangalia.

Mwongozo huu utakusaidia namna ya kutumia maudhui haya kwa njia sahihi, ili kuwezesha uelewa katika jamii na pia kuweza kuchukua hatua juu ya vitu ulivyojifunza.

Kujifunza zaidi kuhusu Uongozi, Uliza TGNP:

WhatsApp: +255752924146 au +255754465306

Barua pepe: monica.john@tgnp.or.tz au neema.mwaisela@tgnp.or.tz

QR code?

KUFAHAMU, MIJADALA, NA VITENDO

Tunaposoma tunaposikia au tunapoona jambo tunapata kujua. Lakini, ili kujifunza, kuelewa, kupata hisia na kubadili mitazamo—tunahitaji kuyafanya kwa vitendo yale tuliyoyasoma, tuliyoyaona au tuliyoyasikia. Tunaweza kufanya wenyewe, kwa kutumia mchezo wa kuigiza au michezo mingine.

Pia tunaweza kuwa na mijadala, kuzungumza na kutafakari na marafiki kuhusu masuala mbalimbali, na kutoa mawazo na mitazamo yetu tukilinganisha na hali halisi iliyopo katika jamii yetu.

TUNAKUMBUKA:

- **10%** ya yale **TUNAYOYASIKIA**
- **20%** ya yale **TUNAYOYASOMA**
- **30%** ya yale **TUNAYOYAONA**
- **50%** ya yale **TUNAYOYASIKIA NA KUYAONA**
- **70%** ya yale **TUNAYOJADILIANA NA WENZETU**
- **80%** ya yale **TUNAYOYAPITIA MAISHANI**
- **95%** ya yale **TUNAYOMFUNDISHA MWINGINE**

Unaweza tengeneza majukwaa ya mijadala ya vikundi kwa ajili ya usomaji, usikilizaji, au utazamaji wa maudhui haya kwa kufuatilia mifano hapo chini, au buni njia bora ya kuwashirikisha wanakikundi.

KLABU YA KUJISOMEA

- Unaweza kuwapatia wanakikundi nakala ya kitabu cha *Kestoria* kinachohusu simulizi za wanawake katika uongozi, wakajisomea kwa wakati wao.
- Kisha tenga muda kwa ajili ya wanakikundi kukutana tena pamoja ili kujadili kile walichosoma. Fuatilia muongozo wa maswali katika ukurasa wa 3, au tengeneza igizo, au majadiliano.

SOMA KWA SAUTI

- Unaweza kutumia wanakikundi wachache kusoma kwa sauti kitabu hicho na wanakikundi wengine kufuatilia. Soma simulizi moja kwa wakati, wanakikundi pia wapatie nakala za kitabu kwa ajili ya kumfuatilia yule anayesoma kwa sauti.
- Kisha jadilianeni kile mlichosikia. Fuatilia muongozo wa maswali katika ukurasa wa 3, au tengeneza igizo, au majadiliano.

TIZAMA VIDEO

- Unaweza pakua video na maigizo na kuyatazama mkiwa kwenye vikundi. Wanakikundi pia wanaweza pakua video hizo na kutizama kwa kutumia simu zao janja.
- Kisha, ongoza mjadala kutokana na kile ulichokiona. Fuatilia muongozo wa maswali katika ukurasa wa 3, au tengeneza igizo, au majadiliano.

KUSIKILIZA

- Unaweza kupakua kestoria simulizi za wanawake katika uongozi zilizopo kwa njia ya sauti na kusikiliza pamoja kama kikundi.
- Nyimbo zinaweza kuchezwa wakati wa mikutano au matukio yenye kuhamasisha au kuongelea ushiriki wa wanawake katika uongozi.
- Kutoa nyimbo hizo kwa familia, marafiki, au majirani ili waweze kuzisikiliza na kupata ujumbe.

A. Mijadala

Mijadala ya wazi: Chagua mtu mmoja katika kikundi atakayeongoza mjadala. Kama kikundi, kubalianeni muda wa kufanya majadiliano na kuuliza.

Kanuni za mijadala ya wazi:
Heshimu mawazo ya wengine, heshimu muda uliotengwa kwa ajili yako, na heshimu wakati mwongozaji akisema kuwa ni muda wa mtu mwingine kuchangia.

Fikiria/Wawili Wawili/Whirikisha:
Kama una watu wengi, unaweza tafta mtu mwingine au kuwapanga watu katika vikundi vya watu 3 hadi 5. Jadili mada husuka kwa dakika 10-15 na kisha warudishe watu kwenye kundi kubwa ili wawasilishe mawazo yao yaliiyotokana.

Andika/Wawili Wawili/Whirikisha:
Watu wanaweza kutumia dakika 10-15 kuandika mawazo yao na uzoefu wao katika hiyo mada. Kisha shirikisha kile vulichoandika kwa mtu moja na kuwa na mjadala mfupi. Baada ya dakika 30, wanakikundi wanaweza kuja kwa pamoja kwa ajili ya kushirikishana yale.

Baadhi ya Maswali Pendekezwa:

1. Simulizi gani imekuhamasisha na kwanini?
2. Kitu gani umejifunza baada ya kusoma/ kuangalia/kusikiliza simulizi?
3. Kutoka kwenye jamii yako, ni jinsi gani wanawake wanashiriki katika uongozi na nafasi za maamuzi?
4. Unafikiri ni vitu gani vinapaswa kufanyika ili kuongeza ushiriki wa wanawake kwenye ngazi za maamuzi kwenye jamii yako au mkoa?
5. Kitu gani kinawashawishi wasichana waweze kujihusisha katika nafasi za maamuzi?
   Kitu gani kinawasaidia kufanikiwa?
   Nini kinafanya wasichana wengi washindwe kushiriki katika nafasi za uongozi?
6. Je! Ni wanawake walioko kwenye uongozi na ngazi za maamuzi kwenye jamii yako wanafanya kazi nzuri?
7. Ni, mchango gani ambao wanawake viongozi wamaefanya katika kuleta maendeleo kwenye jamii yako na mnajisifia?

B. Igizo

Igizo ni moja ya zana zenye nguvu sana katika kutengeneza viongozi. Inatumika kama daraja la kuziba pengo kati ya nadharia na vitendo, inatoa jukwaa huru kujifunza na kukua. Kwa kutumia maigizo, watu wanajenga ujuzi na ujasiri, na kuwa tayari kukabiliana na changamoto wakati wakigombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Kama moja likienda kufanyika vizuri, unaweza kuandaa igizo kwenye jamii ili kuwashirikisha wanajamii baadhi ya nadharia, mawazo yaliyojitokeza katika igizo lenu.

Mawazo ya kutengeneza igizo:

1. Amina anataka kugombea nafasi za udiwani lakini mume wake anamtishia kumuacha akifanya hivyo. Muwe wake ana madai kuwa mara tu wanawake wanapopata vyeo huwa hawawaheshimu.
2. Pendo anashiriki katika mchaka-to wa uchaguzi na anatumia Facebook na Instagram katika kujitangaza. Watu wanaanza kumtumia jumbe za vitisho au za kumdhalilisha kingo.
3. Kutokana na hayo maigizo matatu ya video, tafakari njia mbalimbali za kumaliza igizo lenu.

C. Malumbano

Kwa kujiandaa au kushiriki katika malumbano, unaweza kujifunza na kutumia taarifa kuzipa nguvu hoja zako. Unaweza pia kujifunza namna bora ya kuwasillisha mawazo yako kwa umakini na ushawishi mbele za watu katika kundi. Kupitia kulumbana, unaweza kujifunza kuelewa miti-zamo tofauti na ya kwako, unaweza kuwa na hoja katika kesi ambayo hukubaliani nayo kabisa.

Mchakato

- Kabla ya kuzungumza, mwanamalumbano anatakiwa kujiandaa kwa kukusanya taarifa mbalimbali kwenye mada husika, kutoka maktaba, kwenye magazeti, na kwa kujadiliana na watu.
- Kuwa na timu mbili, mnaweza kuwa na mzungumzaji mmoja, wawili au watatu kutoka kila timu. Timu moja inakubaliana na mada na timu nyingine inapingana na mada.
- Muongozaji atakayeongoza zoezi.
- Muda wa kuongea unagawanywa sawa kwa wazungumzaji katika kila timu.
- Kila mzungumzaji anaongea kile alichojiandaa nacho kutetea upande wake. Upande utakaoanza kuongea ni wa timu inayokubaliana na mada. Zoezi hilo linaenda hivyo hadi wazungumzaji wote wanakamilika. Kila mzungumzaji anakuwa na muda maalumu wa kuongea kwa mfano dakika tatu au tano.
- Kisha malumbano hayo yanaweza kufunguliwa kwa washiriki wengine waliopo, ambapo kila mshiriki atatoa hoja zake aidha kuunga mkono au kupinga mada. Kila kuzungumza kwa mfano dakika moja au tatu.
- Wazungumzaji wanapoongea hoja zao, wanapaswa kuweza kutoa ushahidi au sababu za hoja zao.
    - Sababu zinazotolewa katika mijadala/malumbano ni lazima ziweze kuthibitishwa.
    - Ikiwa kuna hoja zitapingwa, wazungumzaji hawawezi kuja na hoja mpya.
    - Jaji au jobo huchangua timu iliyoshindwa kutokana na ubora.

Mada za Malumbano

Mada pendekezwa za kukusaidia kuanza au unaweza kuja na mada zako kutokana na maudhui.

1. Wanaume ni bora kuliko wanawake.
2. Wanaume wako vizuri sana katika kuingiza vipato/fedha kuliko walivyo wanawake.
3. Kuelimisha watoto wa kiume ni muhimu kuliko kuelimisha watoto wa kike.
4. Hukatisha tamaa kumchagua mtu ambaye unajua atashindwa uchaguzi.
5. Utamaduni hauwezi kubadilika.

D. Mahojiano ★

- Mara baada ya kikundi chako kusoma au kusikiliza maudhui ya ushiriki wa wanawake katika uongozi, baada ya kujadiliana na kubadilishana uzoefu, unaweza kuweka mihadi na chombo cha Habari kwenye eneo lako kwa ajili ya mahojiano ili kuhimiza wanawake kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.
- **Mawasiliano: monica@tgnp.or.tz** ya TGNP kuwasaidia kupata mihadi ya mahojiano na vyombo vya habari kwenye eneo lako husika.
- Unaweza pia kupeleka nyimbo za wanawake na uongozi katika vyombo vya habari na kuwaomba wazicheze katika vituo vyao baada au wakati wa mahojiano.